**Learning by Ear 2010**

**Theme: Illiteracy and education**

**"A GIRL FINISHING SCHOOL"**

**Episode 10:** *"Mafanikio hatimaye"*

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editor**: Yann Durand

**Translator:** Anne Thomas

**Characters:**

**Papa Wali** *(Ana umri wa miaka 55 na ni baba wa watoto watatu-Elinam, Latifa na Souleyman . Anashughulika na karakana ya vyuma lakini hajui kusoma na kuandika. Biashara yake imekuwa ikimwendea vibaya hivi karibuni kwa kukosa vifaa vya kisasa na usimamizi mbaya wa masuala ya kifedha na utangazaji wa kibiashara. Sasa hivi anakaa nyumbani kwa sababu ana matatizo ya macho.)*

**Mamoua** *(Mwenye umri wa 39 , mke wa Papa Wali na mama wa watoto watatu. Hajui kusoma na kuandika na ni mke-nyumbani. Anafanya biashara ndogo ya kuuza uji wa unga wa mahindi mbele ya nyumba yao.)*

**Elinam** *(ana umri wa miaka 23 , mtoto wao Papa Wali na Mamoua, na ni kaka yake Latifa. Ana shahada ya uhandisi. Ameamua kurudi nyumbani kwa wazazi wake kutengeza na kuisimamia karakana ya baba yake. Hata hivyo uamuzi wake kurejea nyumbani umechochewa na mapenzi aliyo nayo kwa Zakia.)*

**Latifa** *(Ana umri wa miaka 19, ni binti yao Papa Wali na Mamoua. Anafanya mazoezi katika zahanati ya maradhi ya macho baada ya kuhitimu kuwa daktari msaidizi. Amekuwa akiishi na kaka yake jijini kwa miaka zaidi ya mitatu)*

**Zakia** *(Mwanamke mwenye umri wa miaka 24, ni mwanamke mwenye uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki wa dhati wa Latifa na ni mkurugenzi wa utangazaji wa shirika lake la Safari za Kitalii na angali akifanya kazi katika mji mdogo ambao yeye na Latifa wanatoka. )*

**Epiphane** *(Ana umri wa miaka 22 na ni mfanyikazi wake Papa Wali. Ni kijana mwerevu sana.Amebadilisha hali ya karakana yao na inaendelea kuimarika, hayo yote ameyatenda kutokana na madarasa yake ya jioni ya kujifunza kusoma na kuandika na pia mafunzo ya ziada aliyopata kuhusu ufuaji vyuma.)*

**INTRO**

**Hujambo na karibu kwenye sehemu ya kumi na ya mwisho katika kipindi cha 'Mtoto wa kike ahitimu " kwenye makala ya Noa Bongo- Jenga Maisha Yako kuhusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.**

*Baada ya kumaliza masomo yake jijini, Elinam amekuwa nyumbani pamoja na wazazi wake kwa yapata miezi minne sasa. Moyo wake umejikita katika mji wao mdogo ambako mpenzi wake Zakia anaishi. Hataki kulaza damu kwa hivyo anaamua kuitengeza na kuisimamia karakana ya babake. Hataki tena kusubiri kuajiriwa na ameamua kutumia ujuzi wake kusimamia biashara ya babake.*
*Mamoua ameridhika sana na hali ya mwanawe huyo wa kiume ingawa hajaufurahia uamuzi wa Elinam kuishi pamoja na Zakia..*
*Binti yake Latifa amesema pia atarudi nyumbani. Amemaliza muda wake wa kufanya mazoezi kwenye Zahanati ya maradhi ya macho na ana taarifa muhimu atakayowajulisha jamaa zake..*
*Jua limeanza kuzama nao Elinam na Epiphane wanajitahidi kumaliza kazi ya upanuzi wa karakana wakisaidiwa na mafundi kadhaa.*
*Hii ni sehemu ya kumi: "**Mafanikio hatimaye!**"na ya mwisho ya makala hii.Tega Sikio!*

## Scene 1, AT PAPA WALI'S WORKSHOP

Elinam na Epiphane

1. **ATMO :** **BUILDING SITE NOISE, MODERATE TRAFFIC**
2. **Elinam:** (**In a loud voice so the builders can hear**) Taratibu na hilo bango tafadhali! Liweke hapo kando tutalisimamisha kesho. (**Shouting**) Epiphane!
3. **Epiphane:** Naam, kaka Elinam?
4. **Elinam:** Niletee kitabu cha orodha tafadhali?
5. **SFX:** **NOISE OF HURRIED STEPS (EPIPHANE)**
6. **Epiphane:** Hiki hapa!
7. **Elinam:** Asante sana! (**Leafing through**)
8. **SFX:** **SOUND OF SHEETS OF PAPER**
9. **Elinam:** Keti hapa kidogo, tafadhali?
10. **Epiphane:** Naam…
11. **SFX:** **PULLING CHAIR, SITTING DOWN (RUSTLE OF CLOTHES)**

12.**Elinam:** (**After some time**) Inatubidi kuweka bei ambayo ni nafuu ukilinganisha na washindani wetu.

13.**Epiphane:** Tayari nimelinganisha bei. Bei yetu ndiyo nafuu zaidi!

14.**Elinam:** Hata hivyo tunaweza kuliimarisha hilo.Hasa tukikataka kujitangaza kuwa sisi ni kampuni mpya inayowafaa watu wasiojiweza kifedha.

15.**Epiphane:** Basi tunapaswa kupunguza gharama ya vifaa tunavyotumia. Inatufaa kununua vitu kwa bei ya jumla ili tupate kwa bei nafuu.

16.**Elinam:** Mbona hatufanyi hivyo? Hilo ni wazo zuri! Tukiwa na uhusiano mzuri na maduka tunayonunua vitu tutapata bidhaa kwa bei nafuu.

17.**Epiphane:** Kweli!

18.**Elinam:** Kutoka sasa utakuwa mkurugenzi wa kiufundi.

19.**Epiphane:** Mkurugenzi wa kiufundi ndiye nani?

20.**Elinam:** Vitu vyote utavisimamia wewe. Vifaa vya kutengeza bidhaa, usimamizi wa mashine na wafanyikazi, utapawa, kufuata na kutekeleza maagizo...

21.**Epiphane:** Hilo ni jukumu kubwa!

22.**Elinam:** Bila shaka, na inakubidi uwe mwangalifu.

23.**Epiphane:** Na wewe utakuwa nani?

24.**Elinam:** Mkurugenzi mtendaji. Majukumu yangu ni uchunguzi wa masoko, huduma kwa wateja, usimamizi wa maswala ya fedha, uuzaji na pia kuhakisha kwamba kampuni inakua na kuongeza utendakazi wake. Hatimaye tutaweza kuwakodishia vifaa wenye sekta ya ujenzi na pengine pia kuanza kutengeza barabara na madaraja.

25.**Epiphane:** Sielewi unalosema, kakangu!

26.**Elinam:** Usijali. Muhimu zaidi ni kwamba wewe Epiphane huwa uko tayari kujifunza mambo mapya mara kwa mara. Wewe ni mwepesi wa kushika mambo!

27.**Epiphane:** Asante!

28.**Elinam:** Nadhani nitawaomba watu watakaojitolea kuja kwenye hafla ya ufunguzi.

29.**Epiphane:** Nina marafiki wengi ambao wanaonekana kupenda hilo jambo. Usiwe na wasiwasi kaka.

30.**Elinam:** Hakuna cha kaka tena, Epiphane. Inatubidi kuanza kufanya mambo kuanza rasmi zaidi, kwa kuwa kampuni yeu imeshakuwa kubwa sasa. Wewe ni mkurugenzi wa kiufundi na mimi ni mkurugenzi mtendaji.

31.**Epiphane:** **(serious)** Sawa, Mkurugenzi Mtendaji!

32.**Elinam:** Ooh! Kumbe muda umekwenda kweli! Watazame wafanyikazi tafadhali! Ninaondoka kwenda kumchukua Bi Zakia.

33.**Epiphane:** Sawa, Mkurugenzi Mtendaji! Tutaonana kesho!

34.**SFX ATMO: SOUND OF STEPS GOING AWAY OUTSIDE TWO PEOPLE (ELINAM, EPIPHANE)**

35.**SFX ATMO: SOUND OF A MOTORBIKE STARTING UP**

## MUSIC

36.**NARRATOR:** B*aada ya siku kadhaa, karakana ilikuwa tayari kwa sherehe za ufunguzi imeshaandaliwa kwa ufungzi rasmi. Elinam amemua kuonyesha shukran yake kwa Zakia kwa kumtambulisha rasmi kwa wazazi wake jioni hii. Mamoua na Papa Wali wamekaa bega kwa bega lakini wana mitazamo tofauti ya mgeni waliyeletewa.*

### Scene 2, AT PAPA WALI'S HOME

Elinam, Zakia, Mamoua na Papa Wali

37.**ATMO: SOUNDS OF THE NIGHT – CRICKETS (FROM THE DISTANCE)**

38.**Elinam: (in a solemn tone of voice)** Wazazi wangu wapendwa, ningependa kuwatambulisha rasmi Zakia ingawa yeye si mgeni katika nyumba hii. Amekuwa rafiki yetu wa dhati kwa muda. Hata wakati mimi na Latifa hatuko hapa alikuwa akitupigia simu kutujulia hali na pia alimletea Baba wateja wapya.

39.**Papa Wali: (interrupting)** Ukweli mtupu! Watu wema kama Zakia hawapatikani kwa urahisi. Kama si yeye, pengine singekuwa hapa leo hii.

40.**Mamoua:** Papa Wali!Mpe nafasi mwanao azungumze mume wangu.

41.**Elinam:** (**Silence**)Sikujua hali ya afya ya baba. Zakia naye pia hakujua kwani lau angejua angetuarifu mara moja. Nilirudi nyumbani kwasababu yake. Nilitaka kushughulikia maswala kadhaa kisha nirejee mjini. Lakini mambo kadha yamesababisha nisalie humu: Afya ya Baba, matatizo ya mama na taasisi ya kukopesha fedha, mustakabali wa Souleyman, ukarabati wa karakana na – muhimu kuliko yote mapenzi yangu kwa Zakia.

42.**Mamoua:** **(nastily?)** Una maana gani unaposema mapenzi kwa Zakia?

43.**Elinam:** Kwanza kabisa niliamua kurejea, kwasababu ya Zakia. Karakana ya Baba imeendelea kudumu kwasababz yake...

44.**Papa Wali:** Ukweli! Mwanao anasema kweli, Mamoua mke wangu.

45.**Elinam:** **(hesitantly)** Ninakiri kuwa zile fedha nilizodai kwamba niliwaletea ili zimlipie Latifa karo zilitolewa na Zakia!

46.**Papa Wali:** **(shocked)** Ati? Unasema nini mwanangu? Zakia alimlipia Latifa karo ya shule?

47.**Elinam:** Kweli, Baba! Sikuwa hata na peni wakati huo. Ingekuwa makosa kumkatizia Latifa masomo. Sasa hivi ni muuguzi hodari.

48.**Papa Wali:** Zakia! Njoo hapa mwanangu! Ebu nikukumbatie !

49.**SFX ATMO:** **SOUND OF CHAIR – SOUND OF STEPS, PAPA WALLI HUGGING ZAKIA**

50.**Elinam:** Zakia alitufaa sana

51.**Mamoua:** **(still with some reluctance)** Alifanya yote hayo kwa nia ya kujipendekeza kwako?

52.**Elinam:** La hasha , Mama. Mimi ndiye niliyembembeleza ili anikubali. Nisingefaulu kwa hilo, ningerudi zangu jijini 'kitambo!

53.**Zakia:** Kwa hisani yetu tusiyarejee yaliyopita. Ninaona haya wakati mnapoyataja. Nilimpenda Elinam tangu tukisoma shuleni pamoja, lakini baadaye sikumtia akilini. Niliridhika na urafiki wangu na mdogo wake.

54.**Papa Wali:** Usijali mwanangu. Mna radhi zetu. Hakuna jambo lolote la kuuzuia uhusiano wenu uendelee.

55.**Mamoua:** Elinam, mimi na babako tutashauriana kuhusu jambo hilo kisha tutakweleza maoni yetu.

56.**Papa Wali:** Haya si mambo ya kushauriana – wape radhi zako.

57.**Elinam:** Asante sana, Baba, Mama, ninawahakikishieni kwamba Zakia hatowavunja moyo. Inanibidi nami nimlipe hisani ya wema wake.

58.**Papa Wali:** Na utayaweza mwanangu! Muhimu zaidi ni kutahadhari usifanye makosa niliyoyafanya mimi babako. Umesoma vyema na utawasaidia wanao kuandama mikondo ifaayo ya elimu.

59.**Elinam:** Asante, Baba!

60.**Papa Wali:** Na wazazi wako wanasemaje, mwanangu?

61.**Zakia:** Wanasema jema letu ni jema lao.

62.**Papa Wali:** Kwanini tusisherehekee haya yote kwa kula chakula kitamu?

63.**Mamoua:** Mhhmmm nishamuelewa babayenu.Hiyo ni ishara kwamba anahisi njaa!

64.**Elinam:** Mimi pia, Mama!

65.**Mamoua:** (**Struggles to get up**) Sawa, Nenda zangu kupika, lakini chakula kitachukua muda.

66.**Zakia**: Mama subiri... Nitakusaidia…twende sote.

67.**SFX ATMO: SOUND OF CHAIRS AND THE STEPS OF THE TWO WOMEN LEAVING THE ROOM**

68.**Zakia**: (**As she leaves, laughing**) Na ikiwa nitafanya hivyo, nitawapigia simu pia!

69.**Papa Wali:** Hongera, mwanangu! Nakutakia baraka kwenye nyumba yako!

70.**Elinam:** Asante Baba.Asante sana kwa kuniunga mkono.

71.**SFX ATMO: NOISE IN THE KITCHEN – POTS AND PANS –RUNNING WATER (IN THE DISTANCE)**

72.**NARRATOR:** *Mamoua ametambua kuwa mke-mtarajiwa wa mwanawe ni mpishi na wote wanafurahia chakula cha jioni. Siku inayofuata Latifa anawasili mapema ili kushuhudia ufunguzi rasmi wa kampuni ya kakake. Baada ya hafla, Zakia anapendekeza kwamba wale chakula cha mchana mlimani ili wapate kuzungumzia siku zao za awali. Elinam anaandamana nao..*

## Scene 3, AT THE RESTAURANT ON THE MOUNTAIN

Latifa, Elinam na Zakia

73.**SFX ATMO: OPEN-AIR RESTAURANT – SOUND OF THE WIND – BIRDS – UNCLEAR VOICES – SOUND OF CUTLERY**

74.**Latifa:** Unasema kwamba Mama ameukubali uhusiano wenu?

75.**Elinam:** Unajua vizuri kwamba Zakia ni mtu mwema!

76.**Latifa:** Una maana kwamba Mama hukubali jambo au kitu chochote au yeyote kinachokuhusu wewe!

77.**Zakia:** Lakini haikuwa rahisi. Nakwambia ukweli!

78.**Latifa:** Hukuogopa?

79.**Zakia:** Nilikuwa tayari kwa kila jambo!Nilikuwa nimejiandaa barabara. Mimi na Elinam tunajua tunachokitaka maishani. Hilo ndilo linalotushughulisha!

80.**Latifa:** Haya, Hongera basi!

81.**Zakia:** Asante sana! Sasa ni zamu yako nawe kutupasha uliyo nayo!

82.**Latifa:** (**Taking her time and clearing her throat**) Haya! Daktari wetu mkuu amewasilisha tatizo la Baba kwa jopo la madaktari wa upasuaji wanaozuru maeneo yote ya nchi. Madaktari hao wanasema watamfanyia upasuaji wa macho. Wanadhani huenda macho ya Baba yakapata nuru.

83.**Zakia:** Habari njema hiyo! Tafadhali, Latifa endelea.

84.**Latifa:** Naam! Haya sasa ni yangu. (**Proudly**) Nimekubaliwa kupata mafunzo kwa kufanya kazi ya kujitolea pamoja na jopo hilo la madaktari wa upasuaji na kutembea pamoja nao duniani kote!

85.**Elinam:** (**enthusiastically**) Hongera! Raha iliyoje! Hapo una matumaini makubwa ya kufanikiwa siku za usoni!

86.**Zakia:** (**With tears in her eyes**) Bahati iliyoje kwako hiyo!

87.**Elinam:** Njoo hapa, dadangu. Njoo nikukumbatie!Asante sana kwa kujiamini hadi hapo!

88.**SFX:** **HUGGING (SIBLINGS)**

89.**Latifa:** Mimi ndiye ninayepaswa kuwashukuru. Isingekuwa nyinyi wawili, singeyapata yote haya niliyoyapata.

90.**Elinam:** Ebu nikubusu wewe pia Zakia! Huu ni ushindi wako!

91.**Zakia:** La hasha, Elinam. Ni ushindi wa elimu!

**OUTRO**

*Elinam, Zakia na Latifa wanakumbatiana huku wakitiririkwa na machozi. Wanakumbuka maisha yao ya siku za awali, matatizo waliokumbana nayo. Shaka, hofu, huzuni, upweke, hasira, mapenzi... Lakini ziada ya yote kuna hisia ya uhuru – hisia kwamba wanayaongoza maisha yao kutokana na ujuzi walioupata tangu walipojiunga na shule- kusoma na kuandika.*

*Na hiyo ndiyo sehemu ya mwisho ya **“Mtoto wa kike ahitimu ”**, mfululizo unaohusu elimu na kutojua kusoma na kuandika ulioandikwa na Frédéric Gakpara.*

*Author: Frédéric Gakpara*

*Editors: Sandrine Blanchard and Yann Durand*

*With the voices of:*

*Technical assistance:*

*Production:*

**Ukitaka kukisikiliza kipindi hiki tena au vipindi vyengine Noa Bongo-Jenga Maisha yako, tazama ukurasa wetu wa wavuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe kupitia anwani:** lbe@dw-world.de

Shukran kwa kuwa nasi muda wote huu.Hadi wakati mwengine kwaheri!

**END OF 10th EPISODE**